

Ili kutatua kero na maswala haya ya kimsingi tunapendekeza:

1. Mipango ya uhamasishaji juu ya sheria na usimamizi wa

na kusini, pamoja na CORDIO (shirika la utafiti na maendeleo ya pwani na bahari ya hindi) na EAWLS(shirika la afrika mashariki la viumbe hai porini) ziliandaa warsha mbili za jamii mwaka 2007/2008 nchini Kenya na Tanzania. Wakilishi wa jamii waliakisi na kuelezea hadhi ya mazingira ya bahari na kutoa mapendekezo thabiti ya kufanikisha rasilimali za bahari na uendeleu wa chuma riziki. Uchapishaji wa brosha hizi ni matokeo ya kazi hiyo.

Warsha za jamii ni sehemu mojawapo ya mradi mkubwa "uhifadhi kiini cha mali kwa chuma riziki katika afrika mashariki" unaofadhiliwa na IDRC (kituo cha kimataifa cha utafiti na maendeleo) na Ford Foundation. Pia mradi wa kujenga uwezo na kuimarisha sera za kuwaezesha jamii ya pwani kusimamia rasilimali zao za bahari katika afrika mashariki unaofadhiliwa na KNCF (mfuko wa fedha wa Kiedanren wa kuhifadhi viumbe). Madhumuni ya miradi hii ni kuongeza maarifa na ufahamu juu ya uhifadhi wa bioanuai unavyochangia chuma riziki na kuwasaidia jamii kudhihirisha umuhimu huu kwa wanasiasa na waundaji sera.

Maoni yaliyotolewa kwa chapisho hili si lazima kuwa mawazo ya mitizamo ya IUCN, IDRC, The Ford Foundation, KNCF, CORDIO au EAWLS.



Ingawa kumekuwa na matukio dhahiri yaliyochangia kuleta mafanikio kwa sekta ya mikoko, mambo yanayofuata bado yanatukera.

1. Ukataji kiholela wa mikoko kutokana na ongezeko la mahitaji ya kuni za tanuru za chokaa zinazomilikiwa na jamii nyingi.
2. Uvunaji haramu wa rasilimali.
3. Doria na tathmini pungufu pamoja na miundo haifu wa msingi ya usimamizi wa kijamii
4. Ukusanyaji wa vyambo vya samaki
5. Mabadiliko ya hali ya anga, mafuriko na mashapo wakati wa El nino
6. Upungufu wa uhamasishaji wa jamii juu ya sheria na sera za misitu pamoja na mpango wa kitaifa wa usimamizi wa mikoko.
7. Kuongezeka kwa misumeno ya kawi na matumizi yake kuvuna mikoko.